**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KALAMBO**

**SHULE YA SEKONDARI CHISENGA**


**Namba za Simu 0746 631 934**

**Mkuu wa Shule 0754 418 957**

**Makamu Mkuu wa Shule 0625 522 286**

**Matron/Patron 0764 879 227**

**Email: chisenga.kalambo@gmail.com**

**Shule ya Sekondari Chisenga**

**S.L.P 752**


**Tarehe 13/06/2023**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ............**

**..................................................**

**S.L.P ......................................**

**..................................................**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI CHISENGA HALMASHAURI YA KALAMBO MKOA RUKWA MWAKA 2023**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023/2024 na atasoma tahasusi ya HGK/HKL

Shule ya Sekondari Chisenga ipo umbali wa Kilometa 103 Kusini Magharibi mwa Mji wa Sumbawanga. Usafiri wa basi kutoka mjini Sumbawanga unapatikana katika kituo cha mabasi cha mkoa (Katumba) Nauli ni Shilingi 5000/= kwa basi.mabasi maarufu yanayoelekea hadi shuleni ni Azuna, Hekima, Mambwe na Ipad yanayoelekea mji maarufu wa Kasanga.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 14/08/2023, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13/08/2023. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/08/2023.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni sketi mbili (2) ndefu na pana ziwe na marinda kumi na mbili (12) rangi ya kijani kibichi na khaki kwa Wasichana na suruali mbili (2) ndefu na yenye upana wa kutosha rangi ya kujani kibichi na khaki, upindo wa chini ugeuzwe juu (turn up) kwa Wavulana [redacted]

ii. Mashati mawawili (2) meupe yenye mikono mirefu

iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama

iv. Sare ya Michezo ni trucsuit moja (1) rangi ya bluu na T- shirt moja (1) rangi ya bluu Raba nyeupeupe jozi moja (1) Kwa wasichana na trucsuit moja rangi ya bluu na raba jozi moja (1) T-shirt ya bluu moja (1) kwa wavulana.

v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

vi. Soksi jozi mbili nyeupe za shule;

vii. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;

viii. Sweta moja la kijani lenye shingo ya **"V"**.

ix. Nguo za kushindia *gauni ndefu mbili* drafti ndogo rangi ya bluu/nyeupe kwa wasichana na suruali nyeusi mbili za kushindia kwa wavulana watakazivalia na T-shirt ya bluu/ ya shule

x. Tai mbili kijani na khaki kwa wavulana na wasichana
xi. Tisheti (T-shirt) moja rangi ya kijivu yenye nembo ya shule inapatikana

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari counter book kumi
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatanishwa*);
iv. Aje na godoro Ft $2^1/_2$ x 6
v. Mashuka rangi ya bluu Jozi 2, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 (*taja rangi);*
vi. Nguo za ndani za kutosha;
vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
viii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
ix. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 2 wa ndani na nje.
x. Bima ya afya NHIF/CHF
xi. Tranker moja (sanduku la chuma)

**2.3 Michango ilipwe kwenye Akaunti ya NMB (62102300132 CHISENGA SECONDARY SCHOOL)**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia

mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA CHISENGA SEKONDARI**

**Saini ya Mkuu wa Shule ...........................................**

**Jina la Mkuu wa Shule JOSEPH R. MAGOGO.**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ..................................**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule JOSEPH R. MAGOGO 0754 418 957**
- **Makamu Mkuu wa Shule MARTINI POLELA 0625 522 286**
- **Mwandamizi Taaluma JESTA KITULILE 0764 879 227**
- **Mwandamizi Malezi HAMISI SHUKURU 0759 540 586**